Uwakili

“Sisi tu wmawakili wa Mungu, tuliokabidhiwa na Yeye wakati, fursa, uwezo, na mali na mibaraka ya dunia na rasilmali zake. Tunawajibika kwake kwa matumizi yake mazuri. Tunakiri umilikaji wa Mungu kwa kutoa utumishi mzuri kwake na kwa wanadamu wenzetu, kwa kumrudishia zaka na kutoa sadaka kwa ajili ya kutangaza injili Yake na kwa kulitegemeza na kulikuza kanisa lake. Uwakili ni upendeleo uliotolewa kwetu na Mungu kwa ajili ya malezi katika upendo na ushindi dhidi ya choyo na tamaa. Wakili huifurahia mibaraka inayowajia wengine kama matokeo ya uaminifu wake. (Mwa.1:26-28; 2:15; 1Nyak.29:14; Hagai 1:3-11; Mal. 3:8-12; 1Kor.9:9—14; Mt. 23:23; 2Kor.8:1-15; Rum.15:26, 27)”

Hakuna kinachoweza kuelezea vema maisha kikristo zaidi ya kujisalimisha – kujitoa kwetu na kumkubali Yesu. Pale tunapomwona Yesu akitoa vyote kwa ajili yetu, huwa tunalia, nimrudishie nini BWANA, kwa ukarimu wote alionitendea? (Zab. 116:12). Tunapotoa vyote kwa Mungu na kwa kweli vitu vyote kwa uhalisi ni vyake (1 Kor.3:21 – 4:2), Mungu huvikubali lakini anatupatia tena ili tuwe mawakili na watunzaji wa vyote tulivyonavyo. Pale tunapomwona Mwokozi akiwa uchi, alivyofungwa, na mgeni, na lile agizo lake la “Basi enendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, (Mt. 28:19), kwa ajili yake tutatafuta kuwa mawakili waaminifu.

Uwakili ni nini?
Kamusi ya Webster inatafsiri wakili ni mtu aliyekabidhiwa nyumba au miliki aitunze. Kanuni ya kutunza hutokana na maelekezo ya mmiliki. Kwa kamusi hiyo hiyo, Uwakili ni kazi au ofisi ya wakili. Umiliki wa Mungu wa vitu vyote ni ukweli wa msingi kwa madai ya kimbingu na ahadi zake, na wa majukumu yote ya mwanadamu. Umiliki ndio hutupatia picha ya uhalisi hata katika mpango wa Mungu kwa kazi yake.

Mungu ni mmiliki: Ushahidi gani wa Bibilia hudhihirisha kuwa Mungu ndiye mmiliki wa vyote? Mungu anamiliki dunia(Zab. 24:1;) Mungu anamiliki bahari (Zab. 95: 5). Mungu anamiliki ng’ombe, hayawani na ndege wa angani (Zab. 50: 9 – 12). Mungu anamiliki fedha na dhahabu (Hagai 2:8); Mungu anamiliki miili yetu (1Kor. 6:19, 20)

Hivyo, twaweza kudai twamiliki mali kadha wa kadha, hata hivyo, kwa ajili ya kazi ya Mungu, hatimaye itakubalika kuwa Mungu hujipatia rasilimali kwa kazi yake kutokana na vile vilivyo vyake. Hatukuja na kitu duniani na hatutaondoka na kitu (1Tim. 6: 7). Vyote vyatoka kwa Mungu na kutokana na vyake, sisi tunamtolea Yeye. (1 Nyak. 29: 14)

Kutambua kwamba Mungu ni mmiliki ni muhimu katika kuleta mapinduzi katika maisha ya kiroho na kutufanya kuelewa uwakili wa mwanadamu.

Mwanadamu ni Wakili
Mt. 14 – 14-30 Mfano wa talanta - wote ni mawakili wa Mungu tuliogawiwa kadiri ya uwezo kwa kila mmoja wetu kulingana na uwezo wetu.
1Kor. 4:2 Wakili anapaswa kuwa mwaminifu
Luk. 12:42 Wakili anatazamiwa kuwa na busara na bidii
Mt. 25: 27 Wakili anatarajiwa kuwekeza rasilimali za BWANA wake

Mt. 21: 34 Wakili anatazamiwa kurejesha mafao kwa BWANA wake Luk. 16:2 Wakili anawajibika kutoa hesabu ya shughuli za uwakili wake Mwa. 2: 16, 17 Wakili anawajibika kuheshimu vile alivyozuilia Bwana wake

Njia za kukiri kuwa Mungu ndiye mmiliki

Maisha yaweza kugawanywa katika makundi ya msingi manne, kila moja ikiwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Mungu ndiye aliyetupatia miili, uwezo, wakati na mali zinazowezekana kumilikika. Hivyo, katika maeneo hayo, kila kundi twaweza kabisa kuonyesha kuwa Mungu ndiye mmiliki.

Uwakili wa miili

Miili tuliyo nayo ni mali ya Mungu. (1 Kor. 6:19 – 20) tumeitwa kula, kunywa au tutende yoyote kwa utukufu wa Mungu. (1 Kor. 10: 31) Watu wa Mungu ni mawakili wao wenyewe pale inapoamriwa: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili yako yote (Luk. 10:27) Kuzitii amri za Mungu, kunachangia afya ya mwili na akili. (Kut. 15:26, Kut. 20: 8-20)

Uwakili wa Uwezo (talanta) Mt. 25: 14 -16

Kila mwanadamu ana uwezo maalumu kiakili na kimwili. Moja aweza kuwa na ujuzi wa uimbaji (muziki) mwingine kuweza biashara na wengine waweza kuwa mafundi wa kushona kwa cherehani au ufundi makenika. Wengine hufanya marafiki haraka, wengine hujichanganya na watu upesi. Kila mtu aweza kuiimarisha talanta alioyonayo kwa utukufu wa Mungu.

Uwakili wa wakati

Zab. 90:12 Basi utujulishe kuzihesabu siku zetu, tujipatie moyo wa hekima
Ef. 5: 15, 16 Kuutambua wakati huleta hekima. Kama Yesu, twapaswa kuwa kwenye kazi ya Baba yetu (Luk. 2:49). "Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo. (Kol.3:23, 24). Katika amri 10 za Mungu, amri ya Sabato huhusu utunzaji wa wakati, kwamba siku sita watu wafanye kazi na siku ya saba wapumzike(Kut.20:8-11) . Mungu ametoa wakati kwa wanadamu wote kwa usawa.

Uwakili wa vile tunavyoweza kuvimiliki

Mungu alipomwumba mwanadamu alimmilikisha vitu. (Mw. 1: 28, 2:15). Alichozuilia, ni kwamba aliweka mti wa ujuzi wa mema na mabaya akaagiza wasile matunda yake. (Mw. 2:16, 17). Baada ya dhambi, wanadamu walipaswa kukumbushwa kwamba Mungu ndiye chanzo cha mema (Yak. 1:17) na kwamba hutupatia nguvu za kupata utajiri (Kumb. 8:18). Kuukumbusha ukweli huu daima, Mungu alianzisha mfumo wa zaka na sadaka.

Swali: Maisha toa mwili, wakati, talanta, mali sawa sawa na nini? Hivyo kuwa wakili ni kutimiza amri ya Mungu ya upendo kwake na kwa wanadamu wenzetu. (Luk. 10:27).

Zaka – Ni sehemu ya saba ya wakati (Kut. 20:9,10) na vitu tunavyopata (Law. 27:30, 32). Mungu anapoagiza tupeleke zaka ghalani (Mal. 3:10) huwa hatuiti tumfanyie upendeleo kwa kuwa zaka ni mali yake.

Iko mifano ya Zaka- Ibrahimu (Mw. 14:20), Yakobo (Mw. 28:20 -20). Waisraeli waliifanya zaka kuwa sehemu ya sheria ya taifa (Law.27: 30-32, Hes. 18: 24, 26, 28 Kumb. 12:6, 11, 17.) Yesu hakuzuia zaka (Mt. 23: 23). Waisraeli wa kiroho hutoa zaka zao kwa Kuhani Mkuu kwa mfano wa Melkizedeki (Hes. 5:9, 10, 7: 1 – 25).

Matumizi ya zaka: (Law. 27: 30,) ni takatifu kwa Bwana. Ni ya kutumika kwenye nyumba ya Bwana (Mal. 3:10. 1Kor. 9:11 – 14). Bwana ameagiza wafanyao kazi ya injili wapate riziki yao kupitia injili. (1Kor.9:11-14). Washiriki wa Kanisa, kwa hiari yao huleta zaka ghalani, ili kiwemo chakula kwenye nyumba ya Mungu (Mal.3:10). Kwa maneno mengine, kwamba ziwepo fedha za kutosha kwenye Kanisa la Mungu kuliwezesha kutoa huduma yake na kupeleka injili kwa kile kiumbe.

Sadaka
Wakristo wakarimu hawatajizuilia michango yao kwa kanisa kwa zaka peke yake. Katika Israeli ya kale, ujenzi wa mahali pa ibada ilipatikana kwa michango ya ukarimu. (Kut. 36:2-7, cf. 1Nya. 29:14.) Sadaka za ukarimu ziliendesha ibada (Kut. 30:12-16, 2Falm. 12:4, 5. 2 Nyak.
24:4 – 13, Neh. 10:32, 33). Wale waliopewa vingi, vitadaiwa kwao pia vingi (Luk. 12:48.) Ukipokea bure, toa bure (Mt. 10: 8.) Hakuna katika agano jipya kunakohafifisha utaratibu wa sadaka.

Ni yakini Waisraeli walimtolea Mungu viwango vinapofikia robo hata theluthi ya mapato yao. Je, kwa kutoa kwao hivyo waliingia kwenye ufukara? Hapana. Badala yake Mungu aliahidi kuwabariki kwa uaminifu wao. (Mal.3:10-12). Tumeitwa kumrudia Mungu atupaye upendeleo (Mal. 3: 7) Tunapoacha, tunaitwa wezi na kulaaniwa (Mal. 3: 8, 9.)

Kinachosalia Baada ya Zaka na Sadaka
Mali yaweza kuwa nguvu ya mema. Mema tunayotendea watu wahitaji, huwa tunamtenda Kristo (Mt. 25: 34 – 40). Dini iliyo safi inajumuisha kanuni ya kuwajali wahitaji katika jamii kwa nafasi zao kama wajane, yatima na kujilinda na dunia pasipo mawaa. (Yak. 1:27). Amhurumiaye maskini, humkopesha BWANA (Mith. 19:17). Kutunza familia ni wajibu na wanaoudharau, hawafai kuliko wasio waamini. (1Tim. 5: 8).

Manufaa ya Uwakili:

Kwa Mtu binafsi – Kwamba tumeonywa kujilinda na choyo kwani uzima wa mtu haupo kwenye vitu alivyo navyo.(Luk. 12:15). Uwakili huongoza kuisulubisha mwili na tamaa zake. (Gal.5:24). Siku moja Yesu atasema “kadiri mlivyowatendea hao, mlinitendea mimi” (Mt.25:40).

Kwa wengine. “Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo, huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.” 1Tim.6:18, 19,).

Kwa kanisa. Kupokea mpango wa Biblia wa uwakili ni muhimu kwa uhai wa Kanisa. Kwa kutoa kwao hulifanya kanisa liwe imara katika kutimiza utume wake na kupeleka injili kwa wote, ili Yesu arudi (Mt. 24:14).